



THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

Gredi ya 7

Mwongozo wa Kutathminia

SEHEMU B na C

SEPTEMBER/OKTOBER 2026

Mwongozo huu una kurasa 10 zilizopigwa chapa

ZOEZI 3: KUSOMA KWA UFAHAMU

1. Majukumu ya watoto hutegemea uwezo na umri wao

Hoja 1x1=1

2. Matokeo ya kutotunza mazingira ni:

- i. Kutakuwa na kiangazi
- ii. Kuenea kwa magonjwa
- iii. Mifugo wataathirika
- iv. Kupungua kwa chakula.

Hoja 1x1=1

3. Namna watoto wanavyochangia kujenga mshikamano:

- i. Wanaposhirikiana na wenzao katika shughuli za usafi.
- ii. Wanaposhirikiana katika shughuli za vikundi.
- iii. Wanapotunza wadogo wao.

Hoja 1x1=1

4. Maana ya kutekeleza ni:

- i. kutimiza
- ii. kufanya
- iii. kutenda

Hoja 1x1=1

5. Kufuata sheria na kanuni zote za shule

Hoja 1x1=1

6. Usimamizi wa shule unafaa kuwajibika kwa:

- i. Kuhakikisha kuwa lango na uzio wa shule ziko imara.
- ii. Kuhakikisha wanaoingia shuleni ni wale walioruhusiwa pekee.
- iii. Kuhakikisha mazingira ya shuleni yako safi.
- iv. Kuwa na vifaa vya kuzimia moto.

Hoja 1x1=1

7. Athari ya kuwa na mazingira chafu:

- i. Kutokea kwa magonjwa
- ii. Uchafuzi wa mazingira
- iii. Wazazi kuwaondoa watoto wao shuleni

Hoja 1x1=1

8. Ni vyema kuchukua hatua mapema.

Hoja 1x1=1

Hakiki majibu ipasavyo.

UFAHAMU WA KUSOMA (READING COMPREHENSION)

UPEO/ALAMA (SCOPE)	KIWANGO CHA UTENDAJI (PERFORMANCE LEVELS)
7-8	4
5-6	3
3-4	2
1-2	1

ZOEZI 4: UFUPISHO

Hoja 1x1= 1

9. Ufupisho wa mambo yanayoonyesha unyanyasaji wa jinsia ya kike katika aya ya kwanza.

Wasichana wanabaguliwa na kunyimwa haki zao za kimsingi. (Maneno 8)

Hoja 1x1=1

10. Athari za dhuluma kwa jinsia ya kike kulingana na kifungu :

Wasichana wanaacha shule, wanatoroka nyumbani na kuathirika kisaikolojia na kiafya (Maneno 10)

11. Ujumbe ufuatao unajitokeza kwenye sehemu iliyokolezwa rangi.

Jamii ielemishwe kuhusu madhara ya mila potofu; ihimize haki na usawa kwa wasichana ili inufaike. (Maneno 15)

Hoja 1x1= 1

12. Maana ya kauli dhiki chungu nzima ni **nyingi, tele au maridhawa.**

Hoja 1x1= 1

UFUPISHO (SUMMARY)

UPEO (SCOPE)	KIWANGO CHA UTENDAJI (PERFORMANCE LEVELS)
4	4
3	3
2	2
1	1

ZOEZI 5: MATUMIZI YA LUGHA

13. B (alama 1)
14. D (alama 1)
15. A (alama 1)
16. C (alama 1)
17. A (alama 1)
18. Nomino ya wingi- Vumbi (alama 1)
19. Kananu anapalilia maua vizuri (alama 1)
20. Kinyume cha neno **Mfalme** ni **Malkia** (alama 1)
21. Babu alipikiwa chai na Nuno (alama 2)
22. Wanafunzi hawatakuwa wakisafisha darasa kesho asubuhi. (alama 1)
23. Jiko ni **Li-Ya** Chumba ni **Ki-Vi** (alama 2)
24. Kitenzi kishirikishi **-ndiye** (alama 1)
25. Sentensi sahili ni zifautazo : (alama 2)
 - i. Baba anasoma gazeti
 - ii. Mama anasakura mtandaoni.
26. Mfano : Kombe la nyanya limerembeshwa. (alama 2)
Jikombe la nyanya limerembeshwa.
27. Kiranja alisema kuwa wangepanda miche ya matunda skiu hiyo jioni. (alama 2)

SARUFI (GRAMMAR)

UPEO (SCOPE)	KIWANGO CHA UTENDAJI (PERFORMANCE LEVELS)
16-20	4
11-15	3
6-10	2
1-5	1

ZOEZI 6 : KUANDIKA (alama 10)

28. Hii ni barua ya kirafiki kuhusu mwaliko.

Muundo wa barua ni ufuatao :

- i. Anwani ya mwandishi.
- ii. Tarehe
- iii. Mtajo.
- iv. Maamkuzi/Utangulizi.
- v. Mwili/Ujumbe
 - Kiini cha mwaliko
 - Tarehe na siku.
 - Matarajio/ratiba
 - Hitimisho/tamati
- vi. Jina la mwandishi.

Viwango vya kutathmini

Vigezo vya kutathmini	Kuzidi matarajio 4	Kufikia matarajio 3	Kukaribia matarajio 2	Mbali na matarajio 1
Sarufi na ufundi wa uandishi	Anadhihirisha umilisi wa kiwango cha juu cha sarufi, uakifishaji na uendelezaji wa maneno katika uandishi wake.	Anatumia sarufi, alama za uakifishaji na kuendeleza maneno ipasavyo katika uandishi. Hata hivyo, ana makosa machache ambayo hayatatizi usomaji.	Ana makosa ya sarufi, uakifishaji na maendelezo ya maneno ambayo yanatatiza usomaji wa sehemu za insha yake.	Ana makosa mengi ya sarufi, uakifishaji na maendelezo ya maneno kuanzia mwanzo hadi mwisho wa uandishi. Msomaji anaweza tu kukisia maana.
Mwandiko	Ana mwandiko nadhifu unaosomeka kwa urahisi.	Ana mwandiko nadhifu unaosomeka kwa urahisi.	Ana mwandiko usio nadhifu lakini unasomeka. Anatenganisha	Ana mwandiko usiosomeka kwa urahisi. Hatenganishi herufi

	Anatenganisha herufi zote ipasavyo kwenye mistari. Anaacha nafasi inayofaa baina ya maneno kutoka mwanzo hadi mwisho wa insha.	Anatenganisha herufi nyingi ipasavyo. Anaacha nafasi inayofaa baina ya maneno.	baadhi ya herufi ipasavyo. Anaacha nafasi zisizolingana baina ya maneno.	nyingi ipasavyo. Anaacha nafasi nyingi zisizolingana baina ya maneno.
Msamiati	Ana uteuzi mzuri wa maneno na matumizi anuwai ya msamiati kulingana na muktadha.	Ana uteuzi mzuri wa msamiati uliotumika kulingana na muktadha.	Anatumia msamiati finyu ambao wakati mwingi haulingani na muktadha.	Anatumia msamiati finyu ambao haulingani na muktadha.
Mpangilio (Muundo na mtindo)	Ana uwiano na mpangilio wa kipekee wa mawazo kuanzia mwanzo hadi mwisho. Amebainisha utangulizi, mwili na hitimisho vilivyo. Anaendeleza mawazo vizuri.	Ana mtiririko wenye mantiki. Kuna uwiano na mfululizo wa mawazo. Kuna utangulizi, mwili na hitimisho. Anaendeleza mawazo vizuri.	Anajaribu kupanga mawazo kimantiki. Utangulizi, mwili na hitimisho hujitokeza kwa kiasi. Anaendeleza baadhi ya mawazo vizuri.	Hana mpangilio unaoeleweka wa mawazo na ni vigumu kufuatilia kazi yake.

Tanbihi : *Kadiria alama za mwanafunzi kwa kuzingatia vigezo hivyo. Jumla ya alama ni 10*

KUANDIKA (WRITING)

UPEO (SCOPE)	KIWANGO CHA UTENDAJI (PERFORMANCE LEVELS)
8-10	4
5-7	3
3-4	2
1-2	1

SEHEMU YA C

ZOEZI 7 : FASIHI (Alama 20)

SEHEMU C

ZOEZI 29

(Alama 10)

a) Mazingira ya shambani.

Sababu za kutaja mazingira ya shambani ni:

- i. Kushika majembe.
- ii. Kung'oa magugu.
- iii. Kutia mbolea.
- iv. Mimea kunawiri.

Tanbihi:

Kutaja mazingira alama 1.

Kuelezea sababu mbili alama 2

Jumla: **Hoja $3 \times 1 = 3$**

b) Ujumbe unaojitokeza katika ubeti wa pili

(alama 2)

- i. Mimea ikitiliwa mbolea hunawiri.
- ii. Jamii hupata shibe mimea inaponawiri.
- iii. Mazao huongezeka na jamii hupata shibe.

c) Mbinu za uwasilishaji wa wimbo huu katika gatu lenu:

- i. Kuimba kwa kuzingatia miondoko ifaayo.
- ii. Kuigiza shughuli zilizomo kwenye wimbo kwa mfano kushika majembe, kung'oa magugu, kuonyesha shibe.
- iii. Kuvaa maleba ya kazi / kutumia vifaa asilia / halisi vya shambani.
- iv. Kuzingatia kupanda na kushuka kwa sauti.
- v. Kuzingatia matumizi ya viziada lugha -ishara za shughuli.

Hoja $3 \times 1 = 3$

d) Sifa za wanajamii wanaoimba wimbo huu:

- i. Wenye bidii.
- ii. Wachangamfu.
- iii. Wenye ushirikiano.
- iv. Wana uhusiano mwema.
- v. Wenye matumaini.

Hoja $2 \times 1 = 2$

30. NOVELA

(alama 10)

a) Suala la uongozi bora limebainika kama ifuatavyo:

- i. Mtemi Makini kutafuta mbinu mbadala za kuimarisha uchumi.
- ii. Kuunda kamati maalumu ya kuchunguza kuwepo kwa madini.
- iii. Mtemi Makini kuwatembelea wananchi kwa nia ya kuleta umoja.
- iv. Mtemi Makini kuunda vikao vya kuwahamasisha wananchi kuhusu umuhimu wa madini.

Hoja $2 \times 1 = 2$

b) Matukio matatu yanayotokana na kugunduliwa kwa madini katika eneo la Baraka

- i. Wapambe kufurahi.
- ii. Wabaraka kupigwa na butwaa kutokana na habari kuwa wangehamishwa.
- iii. Wabaraka kukataa katakata kuhamishwa na kupokea fidia.
- iv. Mtemi Makini kuwatembelea Wabaraka.
- v. Mtemi Makini kuandaa vikao vya kuwahamasisha Wabaraka kukubali fidia na kuhamishwa.
- vi. Wabaraka kukubali fidia na kuhama.
- vii. Maendeleo kuonekana/kupatikana kama barabara na hospitali kujengwa.

Hoja $3 \times 1 = 3$

c) Aina za mandhari

i. Mandhari ya mahali.

- Mkoa wa Machangani.
- Eneo la Baraka.
- Mashambani mwa Wapambe.

ii. Mandhari ya wakati.

- Hatimaye
- hadi leo.
- Wakati huo.
- Baada ya uchunguzi

Hoja $2 \times 1 = 2$

d) Mbinu za lugha

- i. Istiari.-Bidii yao ya mchwa.
- ii. Tashbihi: “Milima ya ajabu iliandamana kama safu ya askari.”
- iii. Methali: Kwa mfano “Hayawi hayawi huwa.” na “Hakuna masika yasiyokuwa na mbu.”

Hoja $3 \times 1 = 3$

FASIHI (LITERATURE)

UPEO (SCOPE)	KIWANGO CHA UTENDAJI (PERFORMANCE LEVELS)
16-20	4
11-15	3
6-10	2
1-5	1



KISWAHILI GRADE 7 ASSESSMENT SHEET: SEHEMU B na C

(Tumia vigezo vya kutathminia ili kurekodi kiwango cha utendaji cha mwanafunzi: 4, 3, 2 ama 1)

		UFAHAMU WA KUSOMA				UFUPISHO				SARUFI				KUANDIKA				FASIHI				MAONI KUHUSU UTENDAJI
NO	JINA LA MWANAFUNZI	4	3	2	1	4	3	2	1	4	3	2	1	4	3	2	1	4	3	2	1	